

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**  
**IDARA YA UHAMIAJI**

ANUANI YA SIMU: "UHAMIAJI"  
TELEFAX: +255 22 112174  
+255 22 2850584  
Email: info@immigration.go.tz



OFISI YA KAMISHNA JENERALI WA UHAMIAJI,  
UZUNGUNI,  
4BARABARA YA MWANGOSI,  
S. L. P. 1181.  
**DODOMA.**  
06 November 2024

---

**TAARIFA KWA UMMA**

**YAH: UTOAJI WA HUDUMA YA VISA ON ARRIVAL KUINGIA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inapenda kuwajulisha wageni na wadau wote kuwa haijasitisha utoaji wa Visa kwa wageni kwenye vituo vya kuingilia na kutoka nchini.

Hata hivyo, Idara ya Uhamiaji Tanzania inashauri wageni wote ambao wanapenda kutembelea Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa madhumuni mbalimbali kuomba Visa kabla ya kuingia nchini kupitia mfumo wa Visa mtandao (e-Visa) <https://visa.immigration.go.tz>. Kuomba Visa kabla ya kuingia nchini mgeni anakuwa na uhakika wa safari yake na hupunguza msongamano na muda wa kuhudumiwa wakati wa kuingia nchini.

Aidha, Idara ya Uhamiaji Tanzania inawahakikishia kuwa inaendelea kutoa huduma bora zenye kukidhi viwango vya Kitaifa na Kimataifa kwa wageni wanaokuja nchini kwa shughuli mbalimbali.

SSI. Paul Mselle

Msemaji wa Idara ya Uhamiaji Tanzania.